



# **GRE TSA UNIVERSITY - THIKA**

## **UNIVERSIY EXAMINATIONS MAY – AUGUST 2018 SEMESTER**

### **BACHELOR OF EDUCATION (ARTS)**

**KODI: KISW 101**

**KOZI: HISTORIA NA MAENDELEO YA KISWAHILI**

**DATE: 6 AUGUST 2018**

**TIME: 3.00 PM – 6.00 PM**

---

#### **MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

1. SEHEMU YA KWANZA **A**: NI YA **LAZIMA**
2. SEHEMU YA PILI **B**: JIBU MASWALI YOYOTE **MATATU**
3. **USIANDIKE CHOCHOTE** KWENYE KARATASI YA MTHANI. KWA KUFANYA HIVYO UTAKUWA UMEVUNJA SHERIA ZA MITIHANI NA UTAADHIBIWA
4. **ANDIKA VIDOKEZO VYAKO NYUMA YA KIJITABU CHA MAJIBU KISHA PIGIA MSTARI BAADAYE**

***TAHADHARI:- Kamera za CCTV zipo kwenye vyumba vyote vya mitihani***

## **SEHEMU YA A: NI YA LAZIMA**

### **Swali La Kwanza**

- a) Wewe ni msimamizi wa jopo la Usanifishaji wa lugha nchini mwako. Ni vipi utaweza kuelekeza kazi hii? **[Alama 10]**
- b) Ainisha lahaja zozote za Pwani ya kati na mifano ya maneno/msamiati au silanbi katika Kiswahili snifu na lahaja husika. **[Alama 6]**
- c) Fasili dhana zifuatazo: **[Alama 5]**
- i) Lahaja
  - ii) Usanifishaji
  - iii) Malengo
  - iv) Masetla
  - v) Mlowezi
- d) “Kiswahili ni lugha ya Kiarabu.” Sanisi kauli hii kwa mapana na marefu kwa kuhimili majibu yako kwa idhibati tosha. **[Alama 10]**
- e) Je, somo hili lina manufaa gani kwako wewekama msomi na mkurufunzi wa Kiswahili? **[Alama 9]**

## **SEHEMU YA B: JIBU MASWALI YOYOTE MATATU**

### **Swali la Pili**

- a) Tathmini uainishaji wa lahaja za Kiswahili. **[Alama 10]**
- b) Jadili kikamilifu malengo ya **L.C.C.** **[Alama 10]**

### **Swali la Tatu**

“Kiswahili ni Kibantu.”Toa kauli yako kuhusu suala hili kwa idhibati tosha. **[Alama 20]**

### **Swali la Nne**

- a) Kiswahili kilianza Kenya, kikakua Tanzania na kisha kufia Uganda. Sanisi kauli hii kwa utondoti na mifano yoyote mwafaka kurutubisha majibu yako. **[Alama 15]**
- b) Ni nini msukumo nyuma ya suala la usanifishaji? **[Alama 5]**

### **Swali la Tano**

- a) Onesha maendeleo ya Kiswahili Afrika Mashariki. **[Alama 10]**
- b) Lugha ya Kiswahili ilienea vipi hadi bara ya Kenya? **[Alama 5]**
- c) Ni zipi changamoto zilizozukz katika harakati za maenezi ya lugha hii ya Kiswahili? **[Alama 5]**

### **Swali la Sita**

a) Eleza namna watu wafuatao walichangia katika maenezi na vilevile kudidimizwa kwa lugha hii al-maarufu Kiswahili katika kanda ya Afrika Mashariki:

i) Wajerumani **[Alama 6]**

ii) Wameshinari **[Alama 6]**

b) Taja lahaja 2 ambazo zilisahaulika katika harakati za uainishaji wa lahaja za Kiswahili.

**[Alama 2]**

c) Mikakati ipi iliyobora inayoweza kutumika katika enzi ya karne hii ya 21 katika

ukuzaji, usambazaji na uimarishaji wa lugha hii ya Kiswahili? **[Alama 6]**

**AHERI**